

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini

TAARIFA KWA UMMA

HUDUMA YA USAFIRI WA DALADALA WAKATI WA MASHINDANO YA KUHIFADHI QUR'AAN UWANJA WA MKAPA - DAR ES SALAAM

Kufuatia uwepo wa mahitaji makubwa ya usafiri kwa ajili ya abiria wanaoenda kwenye Mashindano ya kuhifadhi Qur'aan Tukufu yatakayofanyika tarehe 17/4/2022 uwanja wa Mkapa - Dar es salaam, Mamlaka imetoa ruhusa kwa daladala au mabasi yenye leseni hai za usafirishaji kutoa huduma ya usafiri kwenye uwanja huo kwa masharti yafuatayo:

1. Utozaji nauli usizidi viwango ambavyo vimeidhinishwa na Mamlaka.
2. Safari iwe inaanzia na kuishia katika njia ambayo daladala imesajiliwa kisha kuendelea na safari hadi uwanja wa Mkapa ili kupeleka au kuchukua washiriki.
- Mfano:** Daladala za Tegeta Nyuki - Makumbusho kuitia barabara ya Bagamoyo zitabeba abiria kutoka Tegeta Nyuki hadi Makumbusho, kisha zitaendelea na safari hadi uwanja wa Mkapa na kurudi ili kubeba abiria wa Makumbusho wanaoenda Tegeta Nyuki.
3. Dereva ahakikishe anaafuata sheria zote za usalama barabarani na masharti ya leseni za usafirishaji.
4. Dereva anatakiwa kufuata maelekezo atakayopewa afikapo uwanjani.

Mamlaka inasisitiza watoa huduma kuzingatia maagizo haya, hatua za kisheria zitachukuliwa kwa ye yeyote atakayekiuka.

Imetolewa na;
Mkurugenzi Mkuu,
08 Aprili, 2022.